HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU

MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TARE
04.11.2021 KWENYE KITUO CHA ELIMU STENROOS - DONGOBESH.

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA.**

1. Mh.Joseph.G.Mandoo -Diwani Kata ya Dinamu-M/Kiti H/W-Mwenyekiti.
2. Ndg.A.A.Kuuli -Mkurugenzi Mtendaji (W) -Katibu.
3. Mhe.Petro. S.Tarmo -Diwani kata ya Masqaroda -Mjumbe.
4. Mhe. Ester J. Getagno -Diwani Viti Maalum - Mjumbe
5. Mhe. Nuruana A. Kipapai -Diwani Viti Maalum - Mjumbe
6. Mhe. Rumay Ologa Gidajur -Diwani Kata ya Eshkesh -Mjumbe
7. Mhe.Eliamina Shishi -Diwani Viti Maalum - Mjumbe
8. Mhe.Flatei.G.Massay -Mbunge Jimbo la Mbulu Vijijini-Mjumbe.

**WATAALAM WALIOHUDHURIA.**

1. Ndg.R.Kagaruki -Mweka Hazina (W).
2. Ndg.H.Kolimba -Afisa Utumishi (W).
3. Ndg.J.Kilimba -Afisa Usafi na Mazingira (W).
4. Ndg.M.J.Nduligu -Afisa Mifugo na Uvuvi (W).
5. Ndg.E.Manahiri -Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W).
6. Ndg.A.Mtweve -Mratibu iCHF.
7. Ndg.P.M.Sulle -Afisa Maendeleo ya Jamii (W).
8. Eng.S.G.Bundala -Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W).
9. Ndg.E.Matoke -Kaimu Afisa Ugavi (W).
10. Ndg.F.Simbeye -Afisa Elimu Sekondari (W).
11. Ndg.P.J.Idabu -Kaimu Afisa Elimu Msingi (W).
12. Ndg.G.G.Mwambage -Mwanasheria (W).
13. Ndg.O.Mashelle -Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W).
14. Ndg.S.Sanga -Katibu Tawala (W).
15. Ndg.P.Shirima -Kaimu Mganga Mkuu (W).
16. Ndg.M.E.Nyangisa -Kaimu Afisa Ufugaji Nyuki (W).
17. Ndg.M.Nguvava -Mratibu TASAF (W).
18. Ndg.P.P.Onna -Kaimu Katibu Msaidizi TSC (W).
19. Ndg.K.Laizer -Kaimu Afisa Biashara (W).
20. Ndg.S.K.Kyaruzi -Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W).
21. Ndg.D.Njimba -Kaimu Afisa Usafirishaji (W).
22. Ndg.F.C.Kundy -Afisa Mipango (W).
23. Ndg.T.Yusuph -Mdhibiti Ubora.
24. Ndg.A.R.Audax -Kaimu Afisa Uchaguzi (W).
25. Ndg.M.Mwalyambi -Kaimu Afisa TEHAMA (W).
26. Eng.S.G.Bundala -Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W).
27. Ndg.R.Mwaigaga -Kaimu Afisa Usafi na Mazingira (W).

Scanned with CamScanner

**MAAFISA TARAFA**

1. Ndg.F.Hussein -Afisa Tarafa Daudi
2. Ndg.B.Mwandelile -Afisa Tarafa Haydom.
3. Ndg.U.I.Mghamba -Afisa Tarafa Dongobesh.
4. Ndg.G.L.Nyumainzu -Afisa Tarafa Endagikot.

**SEKRETARIETI**

1. Ndg.H.Mulokozi-Katibu wa Kamati Mwandamizi.
2. Ndg.E.T.Melly-Afisa Malalamiko.
3. Ndg.C.Kajeri -Afisa Utumishi.
4. Ndg.E.N.Samata-Afisa Utumishi.

**WASAIDIZI**

1. Ndg.T.Isaya.

**MUHT.NA.38/FUM/11/2021:KUFUNGUA KIKAO.**

Akidi ya wajumbe ilipotimia Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na kutamka rasmi kufungua kikao mnamo saa 4:49 Asubuhi.

**MUHT.NA.39/FUM/11/2021: KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 22.10.2021.**

Wajumbe waliafiki agenda zifuatazo kujadiliwa katika kikao hicho:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha dondoo za kikao cha tarehe 22.10.2021
3. Kusoma na kupitia muhtasari wa kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha cha tarehe 20.09.2021 na muhtasari wa kikao maalum cha Kamati ya Fedha cha tarehe 21.09.2021.
4. Yatokanayo na kikao cha Kamati ya Fedha cha tarehe 20.09.2021.
5. Taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha mwezi Septemba, 2021.
6. Maombi ya kupatiwa kifungu nje ya ukomo wa bajeti (reallocation between) Tshs. 114,869,115.85 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
7. Taarifa ya manunuzi kwa kipindi cha robo ya kwanza (2021/2022).
8. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha robo ya kwanza (2021/2022).
9. Taarifa ya Idara ya Utawala kwa kipindi cha robo ya kwanza (2021/2022).
10. Taarifa ya utekelezaji Kitengo cha sheria kwa kipindi cha robo ya kwanza (2021/2022).
11. Taarifa ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo uliofanyika tarehe 20 hadi 21 Oktoba, 2021.
12. Maombi ya kupatiwa kifungu nje ya ukomo wa bajeti (Reallocation between) Tshs.950,000,000.00 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.



Scanned with CamScanner

**MUHT.NA.48/FUM/11/2021:TAARIFA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ULIOFANYIKA TAREHE 20 HADI 21 OKTOBA, 2021.**

Taarifa ilitolewa kuwa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ilifanya ziara ya kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu. Ziara hiyo ilikuwa ya siku mbili (2) iliyofanyika tarehe 20 hadi 21 Oktoba, 2021 katika Kata za Maretadu, Hayderer, Endamilay, Haydom, Bashay, Yaeda Chini, Eshkesh, Dongobesh, Masqaroda na Tumati.

Kikao kilipokea taarifa hiyo na baada ya wajumbe kutoa michango mbalimbali ilipitishwa kwa utekelezaji.

**MUHT.NA.49/FUM/11/2021:MAOMBI YA KUPATIWA KIFUNGU NJE YA UKOMO WA BAJETI (REALLOCATION BETWEEN) TSHS.950,000,000.00 KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.**

Taarifa ilitolewa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ilipokea fedha kiasi cha **shilingi 950,000,000.00** katika mwaka wa fedha 2021/2022 nje ya bajeti kwa ajili ya shughuli zifuatazo:-

1) Ujenzi wa madarasa 39 shule za sekondari =**Tshs.780,000,000.00**
2) Ujenzi wa madarasa 4 ya shule shikizi 2 za msingi =**Tshs.80,000,000.00**
3) Ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa Idara ya Afya (3 IN 1)=**Tshs.90,000,000.00**

Kutokana na kwamba fedha hizo hazikuwa kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022, Menejimenti iliwasilisha ombi kwenye Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango ili kuridhia na kupatiwa kifungu nje ya bajeti kwa ajili ya kuwezesha matumizi ya fedha hizo shilingi **950,000,000.00** kama ilivyokusudiwa.

Kikao kilipokea ombi hilo na baada ya wajumbe kutoa michango mbalimbali lilipitishwa kwa utekelezaji.

**MUHT.NA.50/FUM/11/2021:MAOMBI YA KUBADILISHA MPANGO WA MATUMIZI YA TSHS.10,000,000.00 ILIYOBAJETIWA KWA AJILI YA KUCHANGIA UJENZI WA KITUO CHA AFYA MARETADU KWENDA KUCHANGIA UKAMILISHAJI WA HOSTELI 1 YA WANAFUNZI NA NYUMBA ZA WALIMU SHULE YA SEKONDARI MARETADU.**

Taarifa ilitolewa kuwa Kamati ya Maendeleo ya Kata ya Maretadu (WDC) iliwasilisha ombi la kubadilishiwa mpango wa matumizi ya fedha kiasi cha shilingi 10,000,000.00.

Fedha hizo zilitengea kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa kituo cha Afya Maretadu, na hivyo Kamati ya Maendeleo iliomba zipelekwe kukamilisha miradi ya hosteli ya wanafunzi na nyumba nne za walimu.



Scanned with CamScanner

Kwa kuwa kuna watu walikuwa wanaendelea kujitolea katika Halmashuri ya Wilaya ya Mbulu, ilishauriwa watu hao wapewe mikataba ya ajira ili kujaza nafasi husika. Majina yaliyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

1. **Mkadiriaji Majengo (QS)**=QS. Appolon J. Arra
2. **Katibu Muhtasi**=Ndg.Leah Manase Hamay
3. **Afisa Biashara Msaidizi**=Ndg.Anastazia Hhando Basso.

Kikao kilipokea ombi hilo na baada ya wajumbe kutoa michango mbalimbali lilipitishwa kwa utekelezaji.

**MUHT.NA.56/FUM/11/2021: MAOMBI YA FEDHA KIASI CHA TSHS.11,776,193.50 ZA MATENGENEZO KWA AJILI YA GARI STL 3385 LANDROVER STATION WAGON (PUMA) NA SM 10318 LANDCRUISER H/TOP KUTOKA KATIKA BAKI YA FEDHA ZILIZOLETWA KWA AJILI UNUNUZI WA GARI LA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU.**

Taarifa ilitolewa kuwa magari tajwa hapo juu yalifanyiwa ukaguzi na TEMESA na kugundulika yanahitaji matengnezo yatakayogharimu kiasi cha shilingi 11,776,193.50 ambapo gari STL 3385 gharama yake ni Tshs.6,959,758.00 na gari SM 10318 gharama yake ni Tshs.4,816,435.5.

Fedha hizo zitalipwa kutoka katika baki ya fedha zilizoletwa kwa ajili ununuzi wa gari la Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.

Kikao kilipokea ombi hilo na baada ya wajumbe kutoa michango mbalimbali lilipitishwa kwa utekelezaji.

**MUHT.NA.57/FUM/11/2021: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiano wao na kufunga kikao saa 12.21 Usiku.

**ULITHIBITISHWA NA:**

**JINA**......KUULI, A. A........ **JINA**....JOSEPH G. MANDOO....

**SAINI**......[signature]........ **SAINI**......[signature]........

**KATIBU** **MWENYEKITI**

**TAREHE**.....22/11/2021.....



Scanned with CamScanner